OFISI YA RAIS - TAMISEMI

HALMASHAURI YA MJI WA BARIADI

SHULE YA SEKONDARI BARIADI

Barua pepe:
bariadisecondary@gmail.com
Simu:
0754551037/0784989336

S. L. P 423,
BARIADI,
SIMIYU.

KUMB NO: BSS/JIF/F5-2018/5/.....

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BARIADI HALMASHAURI YA MJI BARIADI, MKOWA WA SIMIYU, MWAKA 2018

1 Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha **TANO (V)** katika shule hii kwa masomo ya **tahasusi** ya _____. Lugha ya mawasiliano shuleni ni Kiingereza **TU.** Shule ipo umbali wa kilomita moja (1) kaskazini magharibi mwa mji wa Bariadi Karibu na stendi kuu ya mabasi.

Muhula wa masomo unaanza tarehe _____ Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kati ya tarehe ..... na mwisho wa kuripoti ni tarehe.....

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1 Sare ya shule.

I. Shati (2) mbili nyeupe za tetron za mikono mirefu (long sleev).
II. Soksi nyeupe jozi (2) mbili
III. Viatu vyeusi jozi (2) vya ngozi.
IV. Suruali tatu (3) Khaki (1), damu ya mzee (1) na Nyeusi (1)
V. Fulana (T-shirt) mbili (2) Nyekundu na damu ya mzee zenye nembo ya shule zinapatikana katika duka la shule kwa Tshs 20,000/= zote mbili.

VI. Sweta moja (1) lenye rangi ya damu ya mzee lisiloshonwa kwa mikono

VII. Nguo za michezo Bukta na T-shirt za rangi ya blue (mwanafunzi aje nazo).

VIII. Raba za michezo.

IX. Tai ndefu nyeusi mbili (2)

N.B

1. Mwanafunzi asije na nguo nyingine ambazo sio sare ya shule. Nguo atakazokuwa amevaa wakati wa kuripoti hataruhusiwa kuzivaa mara tu atakapokamilisha sare ya shule.
2. Mwanafunzi anashauliwa kushona suruali baada ya kupewa maelekezo kutoka ofisi ya nidhamu na malezi ili kuepuka kutofautiana katika mashono.

2.2 Ada na Michango ya Shule.

A. Ada ya shule kwa mwaka ni Tshs 70,000/= unatakiwa kulipa yote au Tshs 35,000/= kwa muhula mmoja. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule namba **30501100016 (Bariadi secondary revenue collection)** katika benki ya **NMB.** (Tafadhali andika **jina, kidato na muhula** wa mwanafunzi kwenye Pay in Slip)

B. Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

I. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.

II. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma.

III. Shilingi 30,000/= wapishi, walinzi na vibarua wengine.

IV. Shilingi 10,000/= matibabu.

V. Shilingi 20,000/= mitihani ya Kujipima (mock)

VI. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho.

VII. Shilingi 1,500/= nembo ya shule

michango hii ilipwe kwenye **A/C 30502300027** katika tawi la **NMB**

NB. ADA NA MICHANGO YOTE NI Tshs 177,500/= KWA MWAKA.

C. Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

I. Ream ya karatasi moja - A4 (Kwa mwaka)
II. Vitabu vya masomo ya tahasusi ya kila mwanafunzi.
III. Dissecting kit kwa wanafunzi wa **tahasusi ya PCB**.
IV. Scientific calculator kwa wanafunzi wa tahasusi za **PGM, PCM na PCB**.
V. Godoro dogo ft 2.5 jipya na mto
VI. Picha za pasipoti mbili (2) za rangi andika jina nyuma yake.
VII. Shuka mbili rangi ya pink, blacket moja,chandarua na taulo
VIII. vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kikombe, kijiko –visiwe vya plastiki.
IX. Ndoo mbili (2) ndogo
X. Kwanja moja na jembe.
XI. Mfagio wa ndani na nje.

3. MAKOSA YANAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

I. Wizi
II. Kutohuzuria masoma kwa Zaidi ya siku 60 bila taarifa/utoro
III. Kugoma na kuhamasisha mgomo
IV. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
V. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
VI. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
VII. Uvutaji wa sigara.
VIII. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
IX. Kupata ujauzito, kutoa mimba au kusababisha mimba.
X. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
XI. Kumiliki simu ya mkononi shuleni.
XII. Kudharau Bendera ya Taifa.
XIII. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
XIV. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
XV. kutosoma kwa bidii.
XVI. kuwa nje ya eneo la shule bila ruhusa.

4. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA MWANAFUNZI AWAPO SHULENI:-

I. Kuhudhuria vipindi vya masomo bila kukosa.

II. Kushiriki kikamilifu katika shughuli za usafi wa mazingira kulingana na ratiba ya shule.

III. Kushiriki vyema katika michezo na mazoezi ya viungo.

IV. Kushiriki katika ibada kulingana na imani yake.

V. Kushirikiana na wenzake kikamilifu katika makundi ya kujisomea.

VI. Kuamka asubuhi na mapema kulingana na ratiba ya shule na kushiriki shughuli mbalimbali zilizopangwa kwa siku husika.

VII. Mwanafunzi ataruhusiwa kuwasiliana na mzazi/mlezi wake kupitia simu ya makamu wa mkuu wa Shule na si vinginevyo.

VIII. Mwanafunzi atatakiwa kuvaa fulana ya shule muda wote baada ya masaa ya kawaida ya masomo.

IX. Mahitaji ya kila siku ya mwanafunzi kama vile mswaki, mafuta, daftari, kalamu n.k atayapata katika duka la shule na hataruhusiwa kuomba ruhusa ya kwenda kutafuta mahitaji hayo nje ya eneo la shule.

5. MAMBO MENGINE MUHIMU.

Soma kwa umakini fomu zifuatazo na zijazwe inavyotakiwa.

a) **Medical Examination form** ambayo itajazwa na mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii ikabidhiwe kwa mkuu wa shule mara mwanafunzi atakaporipoti shuleni.

MEDICAL EXAMINATION FORM.

This form must be completed by Government Medical Officer.

Student's full name._____

Age._____ **sex.**_____

- ☑ Blood test. _____ Group _____
- ☑ Stool Examination_____
- ☑ T.S Test_____
- ☑ Asthma_____
- ☑ Eye Disorder_____
- ☑ Ear Disorder_____
- ☑ Nose Disorder_____
- ☑ Anemia_____
- ☑ Chest_____
- ☑ Operations_____
- ☑ Serious accidents_____
- ☑ Any other infection disease_____
- ☑ Pregnancy_____(Females only).

ADDITIONAL INFORMATION. (Physical Impairment, chronic or Family disease e.t.c)

_____

_____

_____

I certify that I have personally examined Mr. / miss_____

And found her/him

fit	unfit

to perform studies.

Signature _____Designation_____

Office stamp

b) Fomu ya mkataba wa Makubaliano kati ya Mwanafunzi/Mzazi/Mlezi) na Uongozi wa shule.

OFISI YA RAIS - TAMISEMI

HALMASHAURI YA MJI WA BARIADI.

SHULE YA SEKONDARI BARIADI.

ANUANI YA MWANAFUNZI/MLEZI

.....

.....

.....

.....

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI BARIADI

S.L.P 423

BARIADI.

YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BARIADI

Mimi

_____

Ambaye ni mwanafunzi niliyechaguliwa kujiunga na kidato cha _____ katika Shule yako. Nakubali binafsi kujiunga na Shule Hii. Naahidi kuwa nitakuwa **mwaminifu, mtiifu** nitafuata **sheria za shule** na nitazingatia taratibu zote za shule, **nitatunza mali zote za Umma** zilizopo hapo shuleni, **nitasoma kwa bidii zangu zote** ili kuiletea sifa nzuri **shule yangu, wilaya, mkoa** na**Taifa** kwa ujumla. Pia nitafanya kazi za shule kwa uwezo wangu wote na **nitaishi kwa amani na kujiheshimu** katika jumuiya ya shule na inayoizunguka shule.

_____

Sahihi ya Mwanafunzi

c) Fomu ya mzazi/mlezi ya kukubali kutimiza mahitaji muhimu kwa mwanangu akiwa shule.

Mimi _____

Mzazi/Mlezi wa _____ Mwanafunzi wa shule ya sekondari Bariadi. Nakubali kutekeleza mambo yafuatayo kwa uongozi wa shule.

i. Mtoto wangu anafika Shuleni na vifaa vyote alivyoagizwa na Shule pamoja na mahitaji yake muhimu.

ii. Kwa kipindi chote Mtoto wangu atakapokuwa mwanafunzi wa Shule ya sekondari Bariadi nitashirikiana na uongozi wa shule kuhakikisha kuwa mwanangu anafuata na kutii sheria, kanuni na taratibu za shule.

iii. Mtoto wangu awapo nyumbani nitampatia muda na mazingira mazuri ya kujisomea.

iv. nitakuwa tayari kufika shuleni mara tu nipatapo wito juu ya masuala ya kinidhamu yahusuyo mwanangu.

v. nitahakikisha kuwa mwanangu anawahi shuleni mara tu likizo inapomalizika.

_____

Saini ya Mzazi / Mlezi.

Namba ya simu ya mzazi/mlezi.....

d). Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi.

picha

HISTORIA YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI.

MAELEZO BINAFSI.

Jina la mwanaafunzi.....

Majina ya wazazi (i) Baba .....hai/amefariki

(ii) Mama.....hai/amefariki

Kabila la mwanafunzi .....dhehebu la dini yake .....

Tarehe ya kuzaliwa ..... sehemu aliyozaliwa .....

uraia wa nchi yake ..... jina la mlezi (kama anatunzwa na mlezi)

.....

Uhusiano na mlezi .....kazi ya mlezi/mzazi .....

Bidhaa au zao analotegemea kama si mfanyakazi .....idadi

ya ndugu katika familia (ke) .....(me) .....

Wategemezi .....ni wangapi wamezaliwa katika familia .....

Afya yako kwa ujumla ..... matatizo ya kudumu ya

kiafya aliyonayo mwanafunzi.....

.....

.....

saini ya mwanafunzi.....

6. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

MWISHO

Karibu shule ya Sekondari Bariadi, ni matumaini yangu kuwa kwa muda wote wa masomo utazingatia nidhamu na kufanya kazi kwa bidii ili uweze kupata mafanikio zaidi kitaaluma.

HONGERA NA KARIBU SANA

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI BARIADI
S. L. P. 423
BARIADI.

DEUS P. TOGA

MKUU WA SHULE

0754551037/0784653966

NAKALA KWA.

1. **Mkurugenzi Elimu ya Sekondari**
   S.L.P 9121
   DAR-ES-SALAAM
2. **Mkaguzi Mkuu wa shule**
   Kanda ya Magharibi,
   S.L.P 1025
   TABORA
3. **Afisa Elimu (M)**
   S.L.P 4,
   SIMIYU.
4. **Afisa Elimu Sekondari (Mji)**
   S.L.P 526,
   BARIADI.